

Bima

Karatasi la uhakika wa muongozo wa pesa zako



Bima ni nini?

Bima husaidia gharama ya kubadilisha vitu kama zikienda vibaya. Kwa mfano:

- ▶ simu yako ya mkono ikianguka chini kutoka mfuko wako na kuvujika wakati unaposafiri na unahitaji kununua ingine mpya
- ▶ wewe ukipatwa na ajali ya gari na unahitaji kutoa malipo kwa ajili ya usaidizi wa dawa na kufanya gari lako itengenezwe.

Hati ya bima ni nini?

Hati ya bima ni mapatano ya kisheria ambapo wewe unalipa pesa kwa mtu anayepatiana bima ili kumwezesha kulipa gharama za kubadilisha au kurekebisha vitu vyako kama kitu kikienda vibaya. Kufanya hivi inakubidi wewe kulipa kiasi cha pesa kinachoitwa premium.

Ni nani anayepeana bima?

Mpeanaji wa bima ni kampuni inayouza bima. Kuna aina tofauti za wapatianaji bima hapa Australia.

Aina za bima

- ▶ **Bima ya gari** hutosheleza gharama ya gari lako kama likiharibika au likiibiwa.
- ▶ **Bima ya Nyumba (bima ya ujenzi)** hutosheleza gharama ya kubadilisha vitu kama kukitokea kitu nyumbani (kwa mfano, uharibifu kutoka moto au kibunga).
- ▶ **Bima ya vitu vya ndani** hutosheleza gharama ya kubadilisha au kutengeneza vitu ulivyo navyo nyumbani kama fenicha, nguo, chombo cha kufanyia kazi na mapambo ya vitu.
- ▶ **Bima ya maisha** hulipia kiasi cha pesa kilichoteuliwa wakati unapokufa. Pesa hizi huenda kwa watu unaochagua wapokee pesa hizo (hii imeandikwa kwenye hati yako ya bima).
- ▶ **Bima ya usafiri** hutosheleza gharama ya vitu fulani kama ukipata shida wakati uko mbali na nyumbani. Kwa mfano: kama ukiwa mgonjwa au ukiumia na kupata matibabu ya dawa; kama ukipoteza kitu na ulazimike kukibadilisha; kama kitu chako kikiibiwa na unahitaji kukibadilisha; au kama mipango yako ya usafiri ikibadilika (kwa mfano, safari yako ya ndege ikifutuliwa mbali).
- ▶ **Bima ya afya** hutosheleza kiasi fulani cha gharama ya matibabu ya dawa kama ukigonjeka au ukiumia.
- ▶ **Bima ya simu ya mkono** hutosheleza gharama ya vitu vingine ambazo zinaweza kufanyika kwenye simu yako (Kwa mfano, kama ikiwacha kufanya kazi au ukiharibu).

Kumbuka

- ▶ Bima ni pesa unazolipa kama vitu vikienda vibaya.
- ▶ Bima hutosheleza gharama ya kubadilisha vitu kama kitu kikitukia.
- ▶ Nchini Australia, kuna vitu vingine ambazo unalazimika kuwa na bima kwake, kama gari lako.

Wapi kupata maelezo

Kwa maelezo kuhusu bima, tembelea tuvuti ya MoneySmart, www.moneysmart.gov.au, au pigia 1300 300 630.



Euly na Apol wanahamia kwenye nyumba mpya

Euly na Apol walifurahia kununua nyumba mpya. Kujitayarisha kuhamia kwenye nyumba yao mpya, walininu a fenicha na vifaa vya umeme vipya kama televisheni na friji. Pia walikuwa na vitu muhimu vya kibinafsi kama mapambo ya vitu na komputa.

Rafiki wa Apol alimwambia yeye apate bima kwa sababu inasaidia kwa gharama ya kubadilisha au kurekebisha vitu muhimu kwako wewe kama kitu kikienda vibaya. Apol alifikiria kuhusu vitu ambazo yeye na Euly walikuwa nazo na jinsi ni muhimu kwao.

Apol aliwasiliana na kampuni mbili za bima ili kudhibitisha gharama sahihi kwa hati ya bima. Alijua kuwa hati ya bima ni kamilifu wakati yeye na mpeanaji bima walipokubaliana kuhusu nini kitawekewa bima.

Kila kampuni ya bima ilimwaambia Apol kuhusu kitu kinachoitwa excess. Hii ndiyo kiasi Apol anacholipa ili kufanya kudai. Apol alijua kuwa kudai ni wakati ambapo anapouliza mpeanaji bima kutoa malipo kwa kitu kilichodhaminiwa na hati ya bima yake.

Apol na Euly waliamua kupata bima ya nyumba (bima ya ujenzi) ili kutosheleza gharama kama wakihitaji kujenga upya au kutengeneza nyumba yao. Pia walininu aina nyingine ya bima – bima ya vitu vilivyo ndani ya nyumba – hii ni dhamana kama vitu vya ndani ya nyumba vimeibiwa au kuharibika. Vitu kama nguo viatu, fenicha, vifaaa na komputa.

Euly na Apol wanafikiria kuhusu aina zingine za bima. Euly alimwaambia Apol kuhusu mama ya rafikiye ambaye ana bima ya afya ambayo inasaidia yeye kulipia gharama za dawa anapokuwa mgonjwa.

Euly na Apol wanafurahia kuwa wanayo bima kwa nyumba yao na vitu vilivyo ndani kama ajali ikitokea au mambo yakienda vibaya. Wanafikiria kuhusu kupata bima ya afya siku za usoni.

This page has been intentionally left blank.